

MIPANGO YA MAENDELEO

TASAF

Manispaa Ya Songea

Issue No. 001

Machi 2017

TOLEO
MAALUM

Ruzuku ya TASAF imeboresha maisha

Soma
Uk.2



Neema kwa kaya masikini Songea

Ruzuku ya TASAF imeboresha maisha

Na Amon Mtega, Songea.

TATHMINI iliyofanywa na timu ya TASAF imeabaini kuwa, ruzuku ya TASAF inayotolewa kwa kaya masikini katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, imebadilisha maisha ya baadhi ya kaya na kuzifanya kuishi maisha bora.

Timuya maafisa wa TASAF hivi karibuni, wakiwa na wanahabari katika ziara ya kutembelea na kukagua kaya masikini ambazo zinapewa ruzuku na TASAF katika kata ya Mjmwema mjini Songea, baadhi ya wananchi waliopata ruzuku hiyo walisema maisha yao yamebadilika kabisa tofauti na hali ambayo walikuwa nayo kabra ya kuanza kupata ruzuku hiyo.

Hawa Hassan (60) mkazi wa mtaa wa kijiweni, kata ya Mjmwema alisema kabla ya

kupata ruzuku ya Tsh.36,000 kutoka TASAF alikuwa anaishi katika mazingira magumu kwa kuwa mume wake alimuacha mara tu baada ya kupata maradhi ya miguu.

"TASAF walipatia ruzuku ya Tsh. 36,000 niliamua kuanza biashara ndogo ndogo ya kuuza mafuta ya kula na nyanya, nilicheza upatu nikapata shilingi laki moja mwezi machi mwaka 2016 nilinunua kuku wa mayai 74, ambao sasa wamekuwa maisha yanaendelea vema", alisema Hawa.

Aidha, alisema hivi sasa ana uhakika wa maisha, hata kama serikali itasimamisha ruzuku inayotolewa na TASAF kwa kuwa miradi yake inaendelea vizuri, na kwamba kuku wake wanaanza kutaga mayai na majogoo aliyonayo anaweza kuuza Jogoo moja hadi Tsh. 20,000.

VITUNGUU

Mkulima, Felix Kajanja ambaye kuitia TASAF amepata mtaji na kuanzisha miradi ya kilimo cha Vitunguu na Mpunga, akipatana bei na mfanyakishara Modesta Mapunda wa Songea.



Naye, Katerina Kayombo(85) mkazi wa mtaa wa kijiweni, Mjmwema alisema tangu ameanza kupata ruzuku ya TASAF maisha yake yamekuwa bora zaidi kwa kuwa zamani alikuwa ombaomba lakini sasa anaweza kupata chakula na kwamba ameanzisha bustani ya mboga mboga ambazo anauza na kujipatia walau kila siku shilingi 2000.

Pia Selina Njelekela(50) alisema kabla ya mradi wa TASAF alikuwa anakula mlo mmoja kwa siku, ambapo hivi sasa ana uhakika wa kula mlio mitatu huku akijishughulisha na biashara ndogo ndogo zinazo mhakikishia chakula kila siku.

Mwingine, Halima Komba(40) alisema kwa miaka mingi alikuwa anaishi katika kibanda kibovu kilicho ezekwa kwa turubai hivyo alikuwa anavujiwa ambapo kuitia mradi wa ruzuku ya TASAF ameweza kuboresha nyumba yake na kuanzisha biashara ndogo ndogo.

Ofisa wa TASAF katika Halmshauri ya Manispaa ya Songea, Kristopher Ngonyani alisema TASAF imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya mpango wa kunusuru kaya masikini kuitia mradi wa TASAF awamu ya tatu lengo likiwa ni kupunguza umaskini kwa watu wasiojiweza.

Awamu ya tatu ya TASAF ilizinduliwa rasmi Agosti 2012 na Rais mstaafu, Jakaya Mrisho Kikwete ambapo Mpango wa kunusuru Kaya Maskini unatekelezwa ili kujenga uwezo na kuwezesha kaya Maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kuboresha maisha.

TASAF Songea yalipa zaidi ya billioni 1 kwa kaya maskini

Na Mwandishi Wetu

TAKWIMU za fedha za TASAF awamu ya tatu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini zinaonesha kuwa kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 zaidi ya shilingi bilioni 1.6 zimelipwa kwa kaya masikini za wakazi wa mitaa 95 ya Manispaa ya Songea.

Ofisa Habari wa Manispaa ya Songea, Albano Midelo alisema hadi kufikia mwezi Mei mwaka 2016, zaidi ya shilingi bilioni 1 na milioni 628 zilikuwa zimepokelewa.

TASAF awani ya tatu ilizinduliwa rasmi Agosti 2012 na Rais mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete ambapo Mpango wa kunusuru Kaya Maskini unatekelezwa, ili kujenga uwezo na kuwezesha kaya Maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu na kuboresha maisha.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari huyo, Katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea uzinduzi wa TASAF awamu ya tatu ulifanyika Januari 5 mwaka 2015 ambapo uzinduzi ulifanywa na mkuu wa mkoa wa Ruvuma wa wakati huo, Said Thabit Mwambungu.

Midelo, alisema Katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2015/2016 kazi mbalimbali ziendelea kufanya ambazo ni kulipa kaya maskini 7,828 kati ya lengo la kaya 7,915 zilizopo kwenye mpango.

Aidha alisema kaya 88 hazikufika siku ya malipo, hivyo fedha zao kurudishwa TASAF Makao makuu kulingana na utaratibu.

Alisema ili kuhakikisha kuwa TASAF awamu ya tatu inafikia malengo yake mfuko umetoa mafunzo kwa Watendaji wa Kata, Wauguzi, Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kuwajengnea uelewa watumishi hao ili wasaidie katika kuondoa umaskini hasa

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo akiwa ofisini kwake



katika kufuatilia masharti ya elimu na afya.

Pia alisema, Mfuko umelenga kutoa elimu kwa kaya maskini kuhusu kilimo cha mazao mbada-la ambayo hayatumii mbolea za viwandani ambapo wananchi hao masikini walifundishwa kilimo cha mazao ya maharagwe, kangan, alizeti, ndizi na mtama.

Alibainisha kuwa, tayari wananchi kutoka kaya hizo masikini walifundishwa kuandaa mbolea ya asili. Mafunzo haya yalifanyika mwaka 2015 katika mitaa ya manispaa ya Songea ikiwemo Mitaa ya Lilambo A, Mwanamonga na Sinai kata ya Lilambo, Mitendewawa, Chandarua na Muhumbezi kata ya Mshangano, Mletele, Non-ganonga na Mdundiko kata ya Mletele, Tanga na Mlete kata ya Tanga, Ndilimalitembo, Mahilo na Chemchem.

Taarifa ya ofisa habari huyo ilieleza pia kuwa timu ya ufuatiliaji ya Wilaya na Mkoa ilifanya ziara kwenye mitaa minne ya Mwengemshindo, Luhira kati, Mitendewawa na Chandarua ili kusikiliza kero za wanufaika wa kaya masikini na kuzitatu.

Uchunguzi uliofanywa na waandishi wa jarida hili, ume-baini kuwa mpango wa TASAF wa kuzinusuru kaya masikini umeleta mafanikio ikiwemo kui-marika kwa mahudhurio ya watoto shule za Msingi na Sekondari, kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kliniki na wanufaika wengi kuanza kujiunga na Mfuko wa Afya wa Jamii.

Baadhi ya wakazi wa Manispaa ya Songea waliipongeza Serikali kwa kuanza mpango huo wa TASAF awamu ya tatu, ambao walisema utaleta manufaa kwa Kaya maskini na kusisitiza tangazo la siku ya malipo liwe linatolewa mapema ili kila mnufaika apate malipo kama inavyostahili, pia kwa Walengwa ambao wata-thibitika kuwa na matatizo kwa siku za malipo, uandaliwe utaratibu maalum wa kuwalipa.

Katika hatua nyingine Taarifa ya idara ya fedha ya Manispaa ya Songea inaonesha kuwa matumizi ya fedha za maendeleo kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 yalikuwa ni zaidi ya shilingi bili-oni nne na milioni 179.

NENO KUTOKA KWA KAIMU MRATIBU TASAF MANISPAA

Mafanikio hayawezi kupimwa mapema, tumejitahidi, tunaendelea

AWAMU ya tatu ya TASAF ilizinduliwa rasmi mwezi Agosti 2012 na Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamuhuri wa Muungano wa Tanzania. Wakati awamu ya tatu, mpango wa kunusuru kaya maskini utatekelezwa ili kujenga uwezo na kuwezesha kaya Maskini kuongeza kipato, fursa na uwezo kwa kugharamia mahitaji muhimu na kuboresha maisha.

TASAF awamu ya tatu ina sehemu kuu nne ambazo ni; kwanza, Mpango wa kunusuru kaya maskini, ambaa una-toa ruzuku kwa kaya maskini sana susani zenye watoto ili ziweze kupata huduma za Elimu na Afya. Pia kutoa aji-ra kwa kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi wakati wa kipindi cha hari na wakati wa majanga mbalimbali kwa mfano ukame, mafuriko n.k, pili Kuongeza kipato kwa kaya maskini kupitia uwekaji akiba na shughuli za kiuchumi ili kuboresha maisha, tatu Kujenga na kuboresha miundombinu inayolenga sekta za elimu, afya na maji, nne Kujenga uwezo katika ngazi zote za utekelezaji.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea uzinduzi wa mpango ulifanyika tarehe 05/01/2015 na Mgeni Rasmi alikuwa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Mhe. Said Thabit Mwambungu. Halmashauri ya Manispaa imetekeleza sehemu ya kwanza mpango huu kwa kuendelea kunusuru kaya maskini 7,915.

Zoezi la ulipaji kaya maskini

Kwa kipindi hiki cha Oktoba hadi Desemba, 2016 Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepokea kiasi cha Shs. 306,882,000.00 kati ya fedha hizo Shs. 272,784,000.00 (88%) ni fedha za walengwa, Tshs 4,649,727.27 (1.5%) sawa na asilimia 1.5 ya walengwa ni fedha zilizoenda ngazi ya mtaa kwa ajili ya usimamizi, Shs 3,099,801.18 (1%) sawa

Afisa Ushauri na Ufutiliaji, Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Aniceth Kyaruzi akiwa anatekeleza majukumu ya TASAF Ofisini kwake.



Kaimu Mratibu wa TASAF, Manispaa ya Songea, Mensa Ngelangela.



na asilimia 1 iliyotumika kwa ajili ya kutoa Elimu ya uanzishwaji wa miradi midogo midogo kwa walengwa na usimamizi wa miradi hiyo ngazi ya kata na Shs. 26,348,454.55 (8.5%) sawa na asilimia 8.5 iliyotumika ngazi ya Halmashauri kwa ajili ya usimamizi na ufutiliaji.

Mafanikio

Mafanikio ya miradi mkubwa na unaohusika wanufaika wengi hayawezi kupimwa kwa muda mfupi, Lakini machache ambayo yameonekana ni kama ifuatavyo;

Mahudhurio ya watoto shule za msingi na sekondari; kwa muda mfupi mahudhurio ya watoto wanaosoma shule za msingi na sekondari yameimarika na utoro wa vipindi umepungua kwa kiasi kikubwa, mafanikio haya yameokana na masharti ya miradi huu ni lazima kwa wanufaika kuhudhuria darasani kwa zaidi ya asilimia 80.

Mahudhurio ya watoto chini ya mka 5; mahudhurio ya watoto chini ya mka 5 kwenye vituo vya kutolea huduma yameongezeka kwa kiasi kikubwa, hiyo ni kutoptaka na sharti la kila mototo chi-

**JARIDA HILI HUTOLEWA
NA HALMASHAURI YA MANISPAA YA
SONGEA MPANGO WA KUNUSURU
KAYA MASIKINI (TASAF)
SLP 14,
SONGEA, RUVUMA.**

BODI YA UHARIRI NA UANDAAJI
Kaimu Mratibu TASAF Manispaa ya Songea: MENSA NGELANGELA
Wahariri: -ALBANO MIDELO- Afisa
Habari Manispaa ya Songea
albano.midel@gmail.com
0784765917
-GREYSON MGOL- Mratibu Ruvuma
Press Club
greysonmgol@gmail.com
0676041181

ni ya miaka 5 anahudhulia kliniki kila mwenzoni.

Kupunguza kero ya wananchi walengwa wa miradi waliondolewa kusongamana mlangoni mwa ofiso ya mkurugenzi na mkuu wa wilaya wakidai wanaomba warudishwe kwenye mpango.

Mafanikio haya yameokana na elimu inayotolewa katika mikutano kuwa endapo unaona hujaridhika kuondolewa basi kata rufaa, lakini kama wewe ni mstaafu au una shughuli yoyote halali ya kukupa kipato kinono basianza mapema kurejesha fedha hizi.

Changamoto za utekelezaji wa miradi na namna zilivyo tatuliwa

Kuhama toka mtaa mmoja hadi mwingine kwa kaya maskini hii inapelekea kutowapata walengwa wakati wa uhakiki na malipo; namna ilivyotatuliwa, wameondolewa kwenye mpango.

Malalamiko kutoka kwa watu ambaa hawapo kwenye mpango wa kunusuru kwaya maskini; watu wengi walikuwa wakilalamika wakati wa zoezi la uhakiki; namna ilivyotatuliwa tumeendelea kuwa elimisha wananchi kutodharau shughuli yeyote inayoleta na serikali kwenye maeneo yao.

Malalamiko kutoka kwa mitaa ambayo haipo kwenye mpango wakidai kutopata ruzuku kama mitaa mengine; namna ilivyotatuliwa, tumewaeleza wananchi kuendelea kuwa na subira mpaaka hapo TASAF Makao watakapota tarifa ya kuibua kaya maskini kwa mitaa iliyobaki.

Malalamiko ya walengwa kuondolewa katika mpango wa kunusuru kaya maskini toka katika mitaa; namna ilivyotatuliwa, Kutoa elimu ya kukataa rufaa kwa yule anayeona anastahili na ameondolewa, lakini kwa yule anayeona anauwezo aanze kurudisha fedha hizo mara moja.

Mhasibu wa TASAF Manispaa ya Songea, Mustapha Mohamed Matili.



Asilimia 29 ya Watanzania ni masikini

Na Albano Midelo

TAKWIMU zinaonesha kuwa asilimia 29 ya watanzania ni masikini na wangepaswa kuingia kwenye mpango wa kaya masikini na kunufaika na TASAF; hata hivyo uwezo wa kifedha wa serikali kutoa ruzuku kwa watu wengi zaidi bado ni mdogo.

Ofisa Habari wa TASAF, Estom Sanga, katika mahojiano maalumu jijini Dar es Salaam hivi karibuni na gazeti la Mtanzania alibainisha kuwa mpango huo umeonesha mafanikio makubwa katika sehemu mbalimbali nchini.

“Mwaka 2013 tulianza kwenda nchi nzima kutafuta walengwa ili kuwapa ruzuku ambayo itawasidia kumudu mahitaji yao ya msingi kama vile chakula, elimu, afya, barabara na maji. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya elimu ni kwamba, watoto kutoka kaya masikini mahudhurio yao shulenii yameongezeka”, anasema Sanga.

Sanga alibainisha kuwa Kabla ya kupata ruzuku, watoto walikuwa wanashindwa kwenda shule kwa sababu ya ukosefu wa sare za shule, daftari, viatu, kalamu, lakini baada ya kupata ruzuku ya TASAF, wanaweza kwenda shule na kupata mahitaji yao muhimu.

Ofisa Habari huyo, alisema ruzuku ya TASAF pia ipo kwenye afya na imewahamasisha watu wengi kupata huduma za afya, ambapo mama mwenye mtoto mdogo amehamasika kwenda kliniki mara kwa mara ili kuangalia afya ya mtoto wake na pia afya yao kama wazazi.

“Hizi ni kaya masikini ambazo zilikuwa haziwezi kupata lishe, walikuwa wanakula mlo mmoja. Idadi kubwa ya walengwa wameweza kuanzisha miradi mdogo midogo ya kiuchumi kama vile kufuga kuku wa kienyeji, nguruwe, kupika maandazi, kuli-ma bustani na kujenga nyumba ndogo ndogo za batii,” anasisitiza.

Hata hivyo, Sanga anasema miradi hiyo ya kujiongeza kipato kiuchumi imeleta mabadiliko kwenye familia zinazopata ruzuku hiyo na kwamba uten-

MGAWO

Wanufaika wa TASAF Mtaa wa Lilambo Manispaa ya Songea wakipata m gavo wa Fedha.



genezaji wa miundombinu kama barabara kwenye maeneo yanayofikiwa na mpango huu umesaidia kurahisisha wananchi kufikia masoko, hospitali na vituo vya afya kwa urahisi.

Mpango huu pia umeweza kwenye walengwa kupata pesa na hivyo kujiamini na kutoka kwenda kwenye mikutano, kwa sababu wameweza kuva nguo nzuri na kanga nzuri na kupendeza.

Anasema wanufaika pia wameweza kuibua miradi mingine ya kimaendeleo kama vile upandaji wa miti, vilevile wamejenga matuta kuzuia maji yasiingie kwenye mashamba yao wakati wa mvua.

Sanga alisema TASAF inahakiki kila wakati wanufaika ili kuhakikisha kuwa wale wanapata ruzuku ya mradi kweli ni walengwa na kusisitiza kuwa uhakiki wa walengwa ni endelevu.

Alisisitiza kuwa zoezi hilo linafanya kila wakati wa kutoa pesa na kila mlengwa anatakiwa awe na kitambulisho ambacho kinatolewa na TASAF na kwamba Kama mlengwa amefariki au hajulikani alipo na haendi kuchukua fedha TASAF wanamuondo kwenye mpango.

Awamu ya kwanza na ya pili, TASAF ilikuwa inajikita kwenye sekta ya elimu, maji, afya, barabara, kilimo, mifugo na shughuli za kiuchumi kama vile

kuweka akiba kwa njia ya vikundi na hivyo kuweza kukopa na kuanzisha au kuendeleza miradi ya maendeleo ambayo itawaingizia kipato na kuwafanya waondokane na umasikini.

TASAF ilianza mwaka 2000, lengo la TASAF ni kuwapa ruzuku walengwa ili kuwajengea uwezo hatimaye nao waweze kushiriki kwenye miradi ya maendeleo na kulipa kodi na hivyo kuchangia pato la taifa.

“Kaya ambazo zipo kwenye mpango ni kaya takribani milioni moja na laki moja na watu waliopo kwenye mpango ni milioni sita, hao ndio walengwa wetu”, anasema Sanga.

Tathmini inaonesha kwamba, kuna mabadiliko makubwa kwenye kaya masikini ambapo walengwa wanapofikia hatua ya kuweza kujimudu, wanaondolewa kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini na wengine wanaingizwa kwenye mpango huo.

Changamoto ni kwamba mahitaji ya watu na idadi ya kaya ambazo ni masikini ni kubwa na uwezo wa Serikali wa kuwapa ruzuku ni mdogo.

Mfuko wa jamii unaotoa ruzuku kwa kaya masikini nchini (TASAF), umekuwa unaotoa ruzuku kwa kaya masikini ili waweze kumudu mahitaji yao muhimu ya kila siku kama vile chakula, mavazi, elimu, afya, barabara na maji safi na salama.

Serikali yashauriwa kufuatilia fedha za TASAF

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI ya Zanzibar imeshauriwa kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha za mpango wa kunusuru kaya maskini(TASAF), ili kujiridhisha iwapo fedha hizo zinawafikia walengwa.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Tanzania Visiwani wameitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufuatilia kwa umakini mkubwa suala la utowaji wa fedha zinazotolewa kwa kaya maskini TASAF ili kuhakikisha fedha hizo zinawafikia walengwa kikamilifu.

Wakichangia ripoti ya kamati ya kusimamia Ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa, Mussa foun Mussa, Bihindi Hamad Khamisi na Suleimani Makame Ali, wamesema kutokana na malalamiko kuwa mengi kwa wananchi ipo haja kwa watendaji wanoshughulikia masuala ya kaya masikini kuhakiki mara kwa mara watu wanaopokea msaada wa TASAF.

Wamesema uhakiki huo uta-

saidia kuwaondoa wasio stahili kupewa ruzuku hiyo, na kuwaingiza wanaostahili kuendelea kufaidika na msaada huo, ambao unasaidia kaya masikini kuinua uchumi wao.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mohammed Aboud, amesema serikali italifatilia kwa kina

suala hilo ili kuwatoa wasio-stahiki na kupisha wanaostahiki kufaidika na msaada huo, na kusisitiza kuwa watu wenye ulemavu watapewa kipaumbele zaidi katika mradi huo ili kuweza kuwasaidia kupata mahitaji yao.

Zaidi ya shilingi bilioni 13.9 zimetumika katika kuzisaidia kaya maskini Unguja na Pemba.

MGAWO

Wanufaika wa TASAF Mtaa wa Sinai Songea wakisubiri mgawo wa fedha.



Wanufaika wa TASAF mtaa wa Ruvuma Chini wakisubiri ku pata ruzuku ya Tasaf,mwezi machi 2017

Wengi wakiri TASAF kuwakwamua na umasikini

Na Greyson Mgoi, Songea.

MARIAM Rajabu, mkazi wa mtaa wa Mabatini anakiri kupata maendeleo makubwa kupidia TASAF, ambapo ameweza kuwasomesha watoto wake watatu, wenye umri wa miaka 16,12 na wa mwisho mwenye miaka mitatu. Mbali na kusomesha watoto, anasema kupidia fedha ya TASAF ameanzisha mradi wa kuuza mboga za majani na anapata kipato cha kumtosha kuendesha familia yake.

“Kabla ya kuanza kupewa fedha hii ya TASAF nilikuwa na maisha magumu, sikuweza kuwa hata na mtaji wa kuweza kununua mbooga za majani kwa bei ya jumla na kuuza kwa jerareja mitaani jambo ambalo saizi nalifanya na linaninufaisha sana”, anasema.

Naye, Sada Hamadi(38), mkazi wa Mtaa wa Mabatini Kata ya Misufini katika Manispaa ya Songea, Mkoani Ruvuma anasema, Serikali kupidia TASAF imemsaidia sana kumkwamua katika lindi la umaskini lililokuwa likimkabili na kumfanya kuishi maisha magumu ye ye na familia yake.

Anasema kabla hajaingizwa katika mpango wa kaya maskini zinazosaidiwa fedha na serikali kujikwamua kimaisha kupidia TASAF, maisha yake yalikuwa magumu, alifanya kazi ngumu ili kujipatia kipato kidogo kuweza kumudu maisha ya kila siku.

Aidha anasema, mara baada ya kuingizwa katika mpango huo mwaka jana, alianza kufanya biashara ya kupika vitumbua vya mchele na kuuza, ambapo alipolipwa fedha ya kwanza alianza na mtaji wa kilo 2 za mchele lakini sasa mtaji wake umekuwa na kumfanya kuwa ananuua kilo 25 za mchele kwa mara moja na kuandaa vitumbua vya kumtosha kwa ajili ya kuuza.

Mama huyo ambaye anakiri wazi kuwa kupidia mradi huo wa vitumbua ameweza kumsomesha mtoto wake, na kumnunulia mahitaji muhimu ambapo kwa sasa yupo kidato cha nne huko Sekondari ya Bombambili katika Manispaa ya Songea.

Pia anatoa wito kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iendelee kuwasaidia watu masikini ili kuwakwamua katika lindi hilo.

“Mimi nawashukuru sana seri-

WANUFAIKA

Wanafunzi mapacha, Catherine na Stephanie komba(15) wanaosoma shule ya Sekondari Londoni iliyopo Manispaa ya Songea, Ruvuma. ambao pia ni wanufaika wa TASAF.



kali, naomba wasituache waendelee kutusaidia ili tuweze kuwalea pia watoto tuliolekezewa na wau-me zetu, kiukweli pesa haitoshi ila inatusaidia kupunguza baadhi ya mambo yanayotukabili”, anasema mama huyo.

Hivi karibuni, akiwa kwenye ofisi za Mtaa wa Mabatini pamoja na watu wa kaya nyingine maskini za mtaa huo, wakisubiri kuja kupokea fedha zao za TASAF, awamu ya 3, Sada anasema anaamini bila kuwa kwenye mpango huo, maisha yake yangekuwa magumu sana na pengine angepata athari za kiafya kutohana na kufanya kazi ngumu mara kwa mara ili kujipatia kipato.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mabatini, Andrew Chilwa amemwambia mwandishi wa makala haya kuwa fedha ya TASAF imesaidia sana kupunguza idadi ya kaya maskini katika mtaa wake kwani wengi wakipata fedha hiyo wanaanza kujishughulisha na biashara ndogo ndogo badee mtaji unakuwa mkubwa wanawenza kujimudu kimaisha.

Anasema katika mtaa wake kupidia kamati ya TASAF walioiunda wamekuwa wakigawana majukumu na kuzunguka kwa tembelea wanufaika, ili kuona wanatumiae fedha hizo ambapo alisema wengi wanatumia kuwashudumia watoto wao wanaosoma, na kuanzisha miradi midogomido go ili kukuza mtaji na fedha hiyo iwasaidia badee.

Anasema katika mtaa wake kwa sasa jumla ya kaya 21 zinanufaika

na TASAF ambapo anasema kabla ya zoezi la uhakiki kufanyika mwishoni mwa mwaka jana, jumla ya kaya 49 zilikuwa zinanufaika.

“Sikujua vigezo gani hasa vilitumika kuwatoa wanufaika wengine kwani kwa jinsi nilivyo ona mimi kuna wengi waliotolewa baada ya zoezi la uhakiki walikuwa wanatakiwa kundelea kusaidiwa kutohana na hali zao duni za kimaisha”, anasema.

Aidha anasema katika mtaa wake kuna wazee maskini wengi ambao wanatakiwa kuendelea kusaidiwa, lakini anashangaa wengine walitolewa kwenye kundi hilo na wengine hawakuandikisha kabisa licha ya kuwa jamii inawaona kuwa wanatakiwa kusaidiwa na serikali ili kumudu maisha.

Ofisa mtendaji wa Mtaa wa Mabatini, Getrude Hiluka anasema kaya zinazonufaika na TASAF sasa ndizo zinazostahili kwani ndizo zilizochaguliwa baada ya zoezi la uhakiki mwaka jana mwishoni, ingawa anakiri kuwepo kwa kaya nyingine nyingi zinazostahili pia, lakini ziliachwa baada ya uhakiki.

“Baada ya uhakiki kaya nyingine ziliachwa na tulipata malalamiko kutoka kwa watu, sasa naomba serikali ikiweza irudi tena katika mtaa wetu kuja kuhakiki kaya nyingine ili kuwaingiza kwenye mpango wa kaya maskini na kuanza kuwasaidia,” anasema.

Taarifa ya Afisa Habari wa Manispaa ya Songea, Albano Midelo inasema kaya maskini 260 kati ya

TASAF imboresha maisha ya kaya masikini Songea

Na Albano Midelo

BAADHI ya wanufaika wa ruzuku inayotolewa kwa kaya masikini katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea Mkao wa Ruvuma wamesema ruzuku imebadilisha maisha, ambapo hivi sasa wana uhakika wa kuishi maisha mazuri angalau.

Wanasema kabla ya ruzuku ya TASAF walikuwa wanakula mlo mmoja kwa siku lakini sasa wana pata milo mitatu na kwamba familia zao zina uhakika wa kusoma elimu ya msingi na sekondari.

Mwajuma Issa (60) mkazi wa Bombambilili Songea ambaye anapata ruzuku ya TASAF ya Tsh.44,000 kila baada ya miezi miwili anasema imemwezesha kuanzisha biashara ya samaki na maandazi hali inayomwezesha kupata fedha za matumizi ya kawaida hivyo kuepuka maisha ya kuombaomba ambayo yalikuwa ya kawaida kabla ya ruzuku ya TASAF.

Mary Milanga (46), mkazi wa Bombambilili ambaye anapata ruzuku ya sh.56,000 anasema amefanikiwa kuanzisha biashara ya pombe ambapo tayari amenunua bati kumi na

KIKAO NI

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Songea Abdul Hassan Mshaweji akizungumza katika moja ya vikao muhimu nya manispaa hiyo.



uwanja katika eneo la Mshangano mjini Songea.

Anasema kwa miaka yote aliku-

wa anaishi katika nyumba iliyozezwa kwa nyasi akivujiwa na mvua kipindi cha masika lakini sasa ana matumaini ya kuingia kwenye nyumba bora iliyozezwa kwa nyasi.

Naye, Kuruthumu Chowo (50), mkazi wa Bombambilili anayepata sh.48,000 anasema ruzuku imemwezesha kuanzisha bustani ya mbooga mboga na kununua kuku kumi wa kienyeji na kwamba analima na mwaka huu amefanikiwa kupata mahindi magunia 15.

Pia, Zulfa Melele (40), mkazi wa Miembeni ambaye anapata Tsh.44,000 anasema ruzuku hiyo imemwezesha kuwa mjasirimali wa kukopesha nguo pia ameweza kuongeza mtaji katika biashara yake na kwamba amefanikiwa kuiniza umeme katika nyumba yake.

Aidha, Emanuel Kayombo (50), mkazi wa Msamala ambaye anapata Tsh.36,000 anasema ruzuku hiyo imemwezesha kuendeleza biashara yake ya pombe,pia fedha hizo amezitumia kununulia chakula,ma-

Inaendelea Uk.9

Wengi wakiri TASAF kuwakwamua na umasikini

Inatoka Uk.7

kaya 2692 zilizoenguliwa katika mpango wa kunusuru kaya masikini katika Manispaa ya Songea zimeandika barua TASAF makao makuu kukata rufaa za kuenguliwa kwao.

Taarifa hiyo anaeleza kuwa kaya 2692 kati ya kaya 7,695 zilizokutwa zinanufaika na ruzuku hiyo zimeenguliwa baada ya uhakiki wa nyumba kwa nyumba kufanyika mwaka jana,ambapo baada ya uhakiki huo kaya zenye sifa zimebakia 5003.

Taarifa ya Midelo Inafafanua kuwa kati ya kaya zilizoenguliwa ilibainika kuwa kaya 1599 katika Manispaa hiyo sio masikini,kaya 342 walihama katika maeneo yao,kaya 110 walifariki,kaya 417 zilibainika kuwa ni hewa na kaya 144 hazikuwepo kwenye uhakiki huo.

Pia inaeleza mara baada ya kaya zilizoenguliwa kupata barua za kuondolewa,yametokeo malalamiko mengi katika kaya hizo hali ambayo imesababisha Manispaa ya Songea kupita katika mitaa ya

walioenguliwa na kutoa elimu ya kukata rufaa kwa wale wanaodhani wameonewa na wale amba wametolewa kihalali kuanza kulipa fedha walizokwisha pewa.

Aidha Taarifa imeeleza kuwa, Kaimu Mratibu wa TASAF Manispaa ya Songea, Mensa Ngerangera amekuwa akitoa elimu kwa nyakati tofauti katika mitaa ya Ruhuwiko Kanisani, Ruhuwiko Shulen, Namanditi, Lilambo A na Sinai na kuwataka wale amba wametolewa kwa kukosa sifa waanze kulipa kama ilivoyelekezwa kwenye barua.

Katika kutoa elimu huko Ngerangera,Amesema kaya maskini ambazo zimeondolewa kimakosa katika mpango huo zinatakiwa kukata rufaa kwa kuandika barua TASAF makao makuu na kwamba ambaye hataandika barua ya rufaa atatakiwa kuanza kulipa deni hilo.

Ngerangera amezitaja sifa za kaya zinazotakiwa kukata rufaa kuwa ni zile ambazo zinakula mlo mmoja kwa siku,kaya isiwe na zaidi ya heka moja,asiwe mfanyakabiashara,mstaafu wala mwenye mtoto au ndugu wa karibu ambaye

ni mtumishi wa umma na asiwe mwenye nyumba bora iliyozezwa kwa bati na kupiga sakafu.

Sambamba na hayo taarifa inabainisha kuwa, Utafiti uliofanika katika baadhi ya mitaa ambayo wameenguliwa waliokuwa wanufaika, umebaini kuwa kuna kaya ambazo zimeondolewa kwa makosa kwa kuwa zina sifa ya kaya maskini,ingawa pia zipo kaya ambazo hazina sifa ya kaya masikini hivyo zinastahili kuenguliwa.

Pia Taarifa hiyo inaeleza kuwa,Ngerangera amesema Novemba-Desemba 2016,kiasi cha Tsh. milioni 277 zilitolewa katika kaya masikini zenye sifa zilizopo katika mitaa 53 ya Manispaa ya Songea ambapo pia Januari-Februari 2017 Manispaa hiyo itatoa kiasi cha Tsh. milioni 256 kwa kaya maskini zenye sifa.

Hivi karibuni Ofisi ya TASAF Manispaa ya Songea imefanya malipo na kutoa elimu katika kaya maskini za mitaa kadhaa ikiwemo mitaa ya; Msafiri, Asiakovu, Pachane, Mabatini, Mfaranyaki, Chandarua, Oysterbay, Tanga, Ruvuma juu na Nonganonga.

TASAF imboresha maisha ya kaya masikini Songea

Inatoka Uki.8

hitaji ya sare za shule, kununua king'amuvi na kuweka sakafu nyumba yake.

Mwingine, Asumpta Milanzi (48) mkazi wa Msamala ambaye anapata ruzuku ya sh.44,000 anasema imemsaidia kuanzisha mradi wa kufuga nguruwe na biashara ndogo ndogo za samaki na dagaa na familia yake inapata chakula milo mitatu na mavazi.

Sambamba na hao, Maria Nigara (35), mkazi wa Msamala ambaye anapata ruzuku ya Tsh.56,000 kila baada ya miezi miwili amefanikiwa kuanzisha mradi wa kuku, nguruwe, kukarabati kisima cha maji na kuweka wawu katika madirisha ya nyumba yake.

Maimuna Somba (41), anayepata ruzuku ya Tsh.52,000 kila baada ya miezi miwili, mkazi wa Msamala amefanikiwa kupiga lipu na sakafu vyumba viwili na kuweka madirisha ya kisasa, kujenga choo na kuongeza mtaji kwenye biashara yake ya pombe.

Esta Mbawala (40), mkazi wa Msamala ambaye anapata ruzuku ya sh.44,000 amefanikiwa kupata milo mitatu kwa siku toka mlo mmoja, analipa pango, watoto wan soma shule na ameanzisha biashara ya dagaa nyasa amba wanampa tia fedha za matumizi.

Melana Soko (55) mkazi wa Lizabon ambaye anapata sh.32,000 anasema amefanikiwa kuanzisha mradi wa kutengeneza majiko ya udongo ya kupikia ambapo fedha hiyo amekuwa anaitumia kununulia udongo, mahindi na kununua mahitaji ya shule kwa mjukuu wake.

Tulizo Goliamma (45), mkazi wa Lizaboni ambaye anapata sh.48,000 amefanikiwa kununua mbolea, mahitaji ya shule kwa wanafunzi, kununua mahitaji ya nyumbani, kulima na kupata mahindi magunia 60.

Halima Tundi(50) mkazi wa Mjimwema ambaye anapata sh.36,000 ameanzisha biashara pombe na kilimo, amefanikiwa kukarabati nyumba na kununua mbolea hivyo kufanikiwa kulima ekari 18 za mahindi.

Teresia Chipeta(47) mkazi wa Ruhuwiko ambaye anapata ruzuku ya sh.36,000 anasema amefanikiwa kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii(CHF) ambapo hivi sasa ana uhakika wa kupata matibabu yeze na familia yake.

Lakini pia anaendeleza biasha-

ra ya pombe, amefuga kuku 10 wa kienyeji, ameezekwa bati nyumba yake, ameanzisha mradi wa kufyatu tofali na kuuza na kwamba sasa ana uhakika wa maisha.

Martha Ambrose(50) mkazi wa Ruhuwiko ambaye anapata sh.40,000 amenunua bati na kueze ka vyumba viwili pia analima na kujipatia chakula na watoto wake wanakwenda shule na maendeleo ya masomo yao yanaridhisha.

Na Mary Barley(42), akishirikiana na mumewe Felix Mkuruah amba wanapata ruzuku ya Tsh.40,000 wakazi wa Ruhuwiko wanasema ruzuku hiyo imewawezesha kuanzisha bustani ya vitunguu ambapo mwezi Oktoba wanatarajia kuvuna gunia tatu ambazo zina thamani ya zaidi ya Tsh.800,000.

Mkuruah akizungumza kwa kujiamini anasema mradi huo utamwezesha kuondoa jina lake katika watu wa kaya masikini wanawezeshwa na TASAF na kwamba nafasi yake ataomba ichukuliwe na mtu mwingine ambaye ni kaya masikini.

"Mara baada ya kuvuna vitunguu na kupata mtaji, mimi sitakuwa kaya masikini tena, nafasi yan-gu nitaomba apewe mtu mwingine ambaye ni kaya masikini, kwa kweli nawashukuru TASAF ndiyo walioniwezesha hadi kufanikiwa kwenye mradi wa vitunguu ambavyo vina soko kubwa", alisisitiza Mkuruah.

Merina Ndumbaro(38) mkazi wa Ruhuwiko ambaye anapata sh.52,000 amefanikiwa kuanzisha biashara ya viazi vya porini(kikande) ambayo kila mwezi mradi huo unamwingizia faida ya sh.60,000, lakini pia ana kuku 25 wa kienyeji na

amefanikiwa kuikarabati nyumba yake kwa kuweka bati na sakafu.

Desdelia Komba(57) mkazi wa Ruhuwiko ambaye anapata sh.32,000 amefanikiwa kuanzisha bustani ya mboga ambayo kila siku inamwingizia kiasi cha sh.8000, lakin pia ameweza kukarabati nyumba yake na amelima mahindi kwa ajili ya chakula.

Mratibu wa TASAF katika manispaa ya Songea Christopher Ngonyani amewapongeza wanufaika wa TASAF ambao wameweza kubadilisha maisha yao kwa kutumia vizuri ruzuku hiyo.

Amesilitiza kuwa lengo la TASAF ni kuhakikisha kuwa wanufaika wote waweze kuendeleza maisha yao hata kama ruzuku ya TASAF utafikia mwisho.

Ngonyani amewaasa wanufaika wote wa TASAF wajitahidi kutumia ruzuku zinazotolewa na serikali kwa malengo yaliyokusudiwa badala ya kutumia kwenye pombe na anasa nyingine.

Halmshauri ya Manispaa ya Songea imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya mpango wa kunusuru kaya masikini kuitia mradi wa TASAF awamu ya tatu lengo likiwa ni kupunguza umaskini kwa watu wasiojiweza.

Hadi kufikia Mei mwaka 2016 zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni 628 zilikuwa zimepokelewa.

Takwimu za mapokezi ya fedha za TASAF awamu ya tatu zinaonesha kuwa kuanzia Julai 2015 hadi Mei 2016 zaidi ya shilingi bilioni 1.628 zilipokelewa na zimeendelea kutolewa kwa kaya masikini za wakazi wa mitaa 95 ya manispaa ya Songea.

WANUFAIKA

Mwalimu Anjelina Chatanda wa Shule ya Msingi Ruhuwiko katika Manispaa ya Songea akiwa na mwanafunzi wake Greysen Kajanja ambaye ananufaika na TASAF.



FELIX KANJANJA, MKAZI WA RUHUWIKO, MANISPAA YA SONGEA


"Mara baada ya kuvuna vitunguu,kuuza na kupata mtaji,mimi sitakuwa kaya masikini tena,nafasi yangu nitaomba apewe mtu mwingine ambaye ni kaya masikini,kwa kweli nawashukuru TASAF ndiyo walioni-wezesha hadi kufanikiwa kwenye mradi wa vitunguu. Natarajia kupata zaidi ya Tsh.milioni 1"


YOSEPHA KOMBA (75), MKAZI WA SINAI, MANISPAA YA SONGEA.

"Nimelima mahindi robo ekari,hata hivyo nakabiliwa na changamoto kubwa ya mbolea na nguvu ndogo ya kupalilia mazao hayo.Pia nalifuga kuku wa kienyeji 30 kutokana na kupata mtaji toka TASAF lakini waliibiwa wote"


STEPHANIA KOMBA (15),MWANAFUNZI WA KIDATO CHA PILI, LONDONI SEKONDARI, MANISPAA YA SONGEA.

"Nashukuru Mpango wa TASAF kuitia mama yangu, Merina Ndumbaro,sasa tunaweza kusoma na kupata mahitaji muhimu ya shule kama vile sare za shule,vifaa vya kuandikia, pia tunapatia milo mitatua kwa siku.Kabla ya kuingia kwenye mpango huu hali ya maisha ilikuwa duni sana,tulikuwa tunakula mlo mmoja kwa siku na vifaa vya shule ilikuwa tatizo kubwa.Katika matokeo ya mtihani wa mwishoni mwa mwaka jana nilishika nafasi ya 16 katи ya wanafunzi 65"


AGNERUS SATU (80), MKAZI WA SINAI, MANISPAA YA SONGEA


"Ruzuku ya TASAF ambayo Tunapata kila baada ya miezi miwili Tsh.36,000,imeniwezesha kuanzisha mradi wa kudumu wa shamba la nusu ekari la kahawa lenye miche 800.Nina matumaini makubwa ya kuondoka katika kaya maskini kwa kuwa zao la kahawa ni la kudumu na mazao yake yanaongezeka kila mwaka, ambapo mwaka huu natarajia kuvuna magunia matatu ya kahawa"


MERINA NDUMBARO, MKAZI WA MTAAWA WA RUHUWIKO KANISANI, MANISPAA YA SONGEA

"Nimetumia ruzuku ya TASAF kuanzisha mradi wa ufugaji wa kuku 25 wa kienyeji,nyumba yangu nimeezeka bati. Kikubwa zaidi nimeanzisha biashara endelevu ya kikande ambacho kinatokana na unga wa viazi vya asili, ambavyo vinapatikana kwa wingi katika wilaya ya Makete,Ludewa na Njombe.Kwa siku ninaingiza hadi Tsh.8000, Inaamini ka debe moja la vikande katika nchi za Zambia na Zimbabwe linauzwa kati ya sh.80,000 hadi 100,000"


CATHERINE KOMBA(15), MWANAFUNZI WA KIDATO CHA PILI, SEKONDARI YA LONDONI MANISPAA YA SONGEA

"Changamoto inayotukabili hivi sasa ni kutembea umbali wa kilometra tano kila siku toka Ruhuwiko hadi sekondari ya Londoni, lakini pia hatuna taa za kusomea usiku hali ambayo inaathiri masomo yetu kwa kiasi flani. Katika matokeo ya mtihani wa mwishoni mwa mwaka jana nilikuwa mwanafunzi wa 33 katи ya wanafunzi wote 65 wa mkondo D wa kidato cha pili"



**MWL.MERINA NDUMBARO WA DARASA LA PILI,
SHULE YA MSINGI RUHUWIKO MANISPAA YA
SONGEA.**

"Maendeleo ya mwanafunzi huyu kabla ya kuingia kwenye mpango wa TASAF hali yake ilikuwa mbaya, muda mwingi darasani alikuwa hana raha, alikuwa hana sare za shule, hata afya yake kwa ujumla ilikuwa inaonekana dhaifu, pia alikuwa hajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Lakini hivi sasa mimi kama mwalimu wake nimeona kuna mabadiliko makubwa ana sare nzuri za shule, viatu, darasani amechangamka, pia sasa anaweza kusoma"



**HAWA HASSANI, MKAZI WA MTAALIWA
MJIMWEMA,MANISPAA YA SONGEA.**

"TASAF imeniwezesha kuanzisha mradi wa kuku 74 wa mayai, ambao naamini baada ya kuza mayai na kuwauza maisha yangu yatakuwa yamebadilika kabisa. Mume wangu alinikimbia na kwenda kuoa mwanamke mwingine, lakini baada ya miezi sita alipokuta nimeanzisha mradi huo, aliomba radhi kwa kunitelekeza. Pia kuititia mradi wa TASAF nimeanzisha biashara ndogo ndogo ambayo inaniingizia fedha na kinifanya kuendesha maisha yangu"



**CATHERINE KAYOMBO(86), MKAZI WA MTAALIWA
MJIMWEMA MANISPAA YA SONGEA.**

"Licha ya kwamba umri wangu ni mkubwa, ninaishukuru sana TASAF kwa kuwa imebadilisha maisha ya kuwa omboomba na hivi sasa kwa kutumia fedha kidogo ambayo ninapewa na TASAF kila baada ya miezi miwili, imeniwezesha kuanzisha bustani ndogo ya mboga, ninauzwa kila siku na naingiza Tsh.3000. Hii kwangu ni fedha nydingi sana, nina uhakika wa kula milo mitatu pia napata mahitaji muhimu ya kila siku, Ahsante TASAF"



**MW.ZABIUNA NCHIMBI,MAKAMU MKUU WA
SHULE YA SEKONDARI YA LONDONI,MANISPAA
YA SONGEA**

"Napongeza mpango wa kusaidia kaya masikini, umesaidia kuboresha elimu kwa wanafunzi ambao wapo katika mpango huo. Hata hivyo nashauri TASAF kuwanunulia vitabu vyao binafsi wanafunzi wanufaika ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa vitabu uliopo katika shule za msingi na sekondari. Shule nydingi za sekondari zinakabiliwa pia na changamoto ya chakula cha mchana. Mfano katika shule zetu wanafunzi wanasona hadi saa 11 jioni, ni vizuri wakapewa chakula cha mchana, nashauri TASAF inagalie pia namna gani watawasaidia vijana hawa kuhusu swala la chakula"



**HALIMA KOMBA, MKAZI WA MTAALIWA
MJIMWEMA, MANISPAA YA SONGEA**

"Nilikuwa naishi katika nyumba iliyozekwa kwa turubai, kwa miaka mingi lakini baada ya kuingizwa katika Mpango wa TASAF wa kunusuru kaya masikini, nimeweza kuezeka nyumba yangu kwa batii, pia ninafanya biashara ndogo ndogo, watoto wangu wana sare na familia yangu kwa ujumla ina uhakika wa milo mitatu kwa siku"



**DESDERIA KOMBA(60), MKAZI WA MTAALIWA
RUHUWIKO KANISANI MANISPAA YA SONGEA.**

"Ninapata Tsh.32,000, TASAF imeniwezesha kuanzisha bustani ya mboga ambayo kila siku inaniingizia kiasi cha Tsh.8000,lakini pia nimeweza kukarabati nyumba yangu na nimelima mahindi kwa ajili ya chakula"



UMASKINI

Afisa Habari wa Manispaa ya Songea, Albano Midelo akizungumza na mmoja wa wazee kutoka kaya ya masikini.

**WANUFAIKA**

Baadhi ya wanufaika wa TASAF Manispaa ya Songea wakisubiri mgawo wa fedha za TASAF.

**MLEMAVU**

Betha Haule(75),Mkazi wa Mtaa wa Ruhuwiko kanisani Songea,ni mlemavu,hana nyumba,anakula mlo mmoja kwa siku hapa ndipo anapoishi,ni mionganii mwa wanufaika wa TASAF

**KAYA**

Baadhi ya Kaya Maskini katika Mtaa wa Sinai Manispaa ya Songea wakipata elimu kuhusu TASAF

**WAZEE**

Baadhi ya wazee kutoka kaya masikini,Manispaa ya Songea.

**UFUGAJI**

Bibi Hawa Hassan Mkazi wa Mtaa wa Mjimwema Songea akiwa na mradi wake wa kuku 74 wa mayai baada ya kupata ruzuku ya TASAF.



KIKANDE

Merina Ndumbaro Mkazi wa Songea ambaye ruzuku ya TASAF imemwezesha kuanzisha mradi wa bishara ya Kikande inayomwingizia Tsh.60,000 kwa mwezi

**UMASKINI**

Kaimu mratibu wa TASAF manipaa ya songea,Mensa Ngelangela alipotembelea kaya masikini Mtaa wa Lilambo A Manispaa ya Songea.

**MGAWO**

Wanufaika wa TASAF mtaa wa Oysterbay Manispaa ya Songea wakisubiri kupata mgawo wa Ruzuku.

**RUZUKU**

Halima Komba,Mkazi wa Mtaa wa Mjimwema,Songea alikuwa anaishi nyumba ambayo ilikuwa imeezekwa kwa turubai,baada ya kupewa ruzuku na TASAF ameezekwa batii

**MBOGA**

Katherima Kayombo(85) mkazi wa Mjimwema Manispaa ya Songea ambaye TASAF imemwezesha kuanzisha mradi wa mboga za majani

**MAHARAGE**

Mama mnufaika wa TASAF Mnispaa ya Songea akichambua maharage yake aliyolima mara baada ya kupata fedha ya TASAF.





TANZANIA SOCIAL ACTION FUND

MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII

Songea, Tanzania

Tel: (025)2602970

FAX: (025)2602474

Email: songea.municipal@gmail.com